# *UKOMBOZI*

**Na mchungaji Chuck**


## NENO LA LEO

**SADUKU LA POSTA 8000 COSTA MESA CA 92620**

**w.w.w. twft.com**

**Kwa yule aliyetukomboa kupitia damu yake Msamaha wa dhambi kulingana na utajiri Neema yake na**

# Waefeso 1:7

## UKOMBOZI

Katika kitabu cha Waefeso 1, Paulo anashukuru kwa ajili ya vipawa vya Roho Mtakatifu. Hayo mambo ni ya muhimu sana na nilazima yawekwe maanani na ni kwa sababu ya wahubiri ambao wanaofundisha sana kuhusu mambo ya kidunia na kuacha mambo ya kiroho. Ndugu wa kiroho yeye hushuhulika na mambo ya kiroho lakini mtu wa kimwili hushuhulika na mambo ya kimwili. Tukihesabu hizi baraka, Paulo anaelekeza kidole kwa Yesu Kristo ambaye ametukomboa na damu yake (Waefeso 1:7). Katika tamanduni zetu hatuna ufahamu kamili wa hili neno ukombozi na kwa hivyo kukosa shukurani ya vile Yesu alitufanyia msalabani.

Neno ukombozi lina mizizi yake ndani ya agano la kale ambapo lina hamanisha ya kwamba, kukomboa mali kwa kulipa gharama yake. Kulingana na mila na utamanduni wa wayahudi, myahudi angeuzwa kama mtumwa na kutumika miaka sita na mwaka wa saba angewekwa huru. Huu mwaka unahitwa mwaka wa ukombozi. Kama angewekwa huru kabla hiyo miaka kuisha, mwenye mtumwa angelipa ile miaka iliyosalia. Pia huu mpangilio unaonekana hata kwa kuhuza mali ama mashamba. Mpango huu hulikuwa mzuri kwasababu mali ingebakia kwa ukoo na kwahivyo yule mtu angekomboa hii mali angeitwa “Goel” yaani mkombozi. Kitabu cha mambo ya walawi 25:

Mfano mzuri unapatikana katika kitabu cha Ruthuu. Katika hadithi hii tunasoma juu ya jamii moja ya Elimelech (tafsiri yake Mungu ni mfalme) na Naomi (tafsiri yake mzuri) walikuwa wanahishi Yerusalemu. Wakati wa kiangazi walihuza shamba yao na kwenda nchi ya Moab na watoto wake wawili wa kiume, Mahlon (tafsiri yake ni mgonjwa) na chilioni. Mtoto wao wa kwanza alikuwa mgonjwa na yule wa pili alionekana na afadhali kidogo.

Baada ya kuishi Moab kwa mda, Elimelech alikufa na wanawe wa kiume ambao walikuwa wameoa wanawake wa Moab wakafa pia. Baada ya vifo vya wanawe, Naomi aliwatangazia bibi za watoto wake madhumuni yake ya kurudi nyumbani kwao. Kwa watu wao. Na akawambia wanaweza kurudi kwao na kuolewa tena ili wakapate furaha. Mmoja wa wale wasichana kwa jina Orpha alilia kwa uchungu na kumuanga mama yake. Lakini Ruthuu kwa moyo mkuu akasema Ruthuu 1:16-17.Usinisihi nikuache, nirejee nisifuatane nawe. Maana wewe uendako nitakwenda, nawewe ukaapo nitakaa watu wako watakuwa watu wangu, pale utakapo kufa nitakufa nami. Na papo hapo nitazikwa. Bwana anitendee vivyo hivyo na kuzidi ila kifo tu kitatutenga wewe na mimi.

Kwa hivyo Ruthuu na Naomi walirudi Betheleemu. Basi walipofika Bethleemu marafiki wao waliwakaribisha na shangwe na deremo. Naomi akawambia msiniite mzuri bali mniite machungu kwasababu Bwana amenitenda machungu. Ruthu 1:20.

Katika kitabu cha kumbu kumbu la torati 24:19 uvunapo mavuno yako katika shamba lako ukasahau mganda shambani, usirudi kuuchukua na uwe wa mgeni au yatima, au

mjane, ile Bwana  Mungu wako, akubariki katika kazi yote ya mikono yako. Mungu alipenda wana wa Israeli wakakubuke shida walizo zipata Msiri na kwa hivyo wakawe na huruma kwa wale hawana.
Kwa hivyo Ruthuu alijitolea kwenda kuokota chakula kwa yale mashamba na kujikuta kwa shamba la Boazi ambaye ni wa ukoo wa Elimelech. Wakati wa adhuhuri Boazi alikuja kuangalia kazi yake na hapo akamuona Ruthuu. Akauliza ni msichana wa nani huyu mrembo?.
Alipogudua ni Ruthuu kutoka nchi ya Moab, mkaza mwana wa Noami alimkaribisha kwa shamba lake na ale na anywe kwenye mitungi ya wafanyikazi wake. Ruthuu alishangaa ule uzuri Boazi alimtendea na akauliza, na Boazi akamuambia kwamba amesikia ule uzuri alimtendea Naomi.
Kwa hivyo Ruthuu aliporudi nyumbani, Naomi alishangazwa na chakula kingi Ruthuu alileta, akamuhuliza na Ruthuu akamuambia alirokota kwa shamba la Boazi. Naomi akamwambia kuwa Boazi alikuwa mtu wa ukoo wao kumbuka kwa kihibrania nen 'kinsman.' Ama 'Goel' inahamanisha mkombozi. Mtu wa ule ukoo ambaye ungelipa ili gharama kwa kukomboa mali ama mtumwa.
Wakati wa mavuno ulipoisha, Naomi alimwambia Ruthuu angalie pale Boazi anapolala. Na Ruthuu alienda na kulala miguuni pa Boazi. Na Naomi alijua ya kwamba Boazi angelijua la kufanya. Katika utamaduni wa wayahudi, kama mtu angeoa halafu afe bila wototo, ndugu yake angemchukua yule mke ili amzalie ndugu yake watoto. Ili hakadumishe jina la ndugu yake katika nchi ya Israeli. Mambo haya yamefanywa katika kitabu cha mwanzo 38 kuhusu vijana wa Juda na Tamari.  Ikafanywa sheria katika kitabu cha kumbu-kumbu la torati 25: 5-10.
Pia katika kitabu cha Mathayo 22:23, masadukayo wakamuhuliza Yesu, kama watu saba wakioa mwanamke mmoja. Mwisho huyo mwanamke akifa akifufuka atapewa jina la nani? Yesu akawambia, watu wakifufuka watakuwa kama malaika akuna cha kuoana. Mathayo 22:30.

Sheria katika kitabu cha kumbu-kumbu la torati 25 ulitoa nafasi kwa ndugu kupeana majukumu yake angeleta kiatu chake na kumpea huyo mwingine ama hivyo dada na dada angemtemea mate kwa uso. Kwa hivyo huyo ndugu angewekwa huru kwa yule

aliyepeana kiatu angepewa jina la kudharauliwa. Kumbu-kumbu la torati 25: 5-10.

Kwa vile watoto wa Elimelich walikuwa wamekufa, kulikuwa akuna mtu angendeleza jina lake. Kile Ruthuu alichokifanya wakati alijifunika blanketi la Boazi ni kusema anataka waoane. Boazi alifurahi sana maana alimpenda Ruthuu sana. lakini kulikuwa na mtu mwingine wa ukoo wa Elimelich ambaye alikuwa ndiye kisheria angemuoa Ruthuu. Boazi akampa chakula Ruthuu akamwambia arudi kwa Naomi. Ruthuu alipomueleza Naomi. Naomi alimuambia asijali maana Boazi atashughulikia hayo mambo. Kesho yake Boazi na wazee waliketi wakizungumza na yule ndugu akapita na Boazi akamuambia kuwa kuna shamba la kukombolewa na akakubali.

Lakini akamwambia lazima amuoe Ruthuu, ili akamzalie mtoto nduguye aliyefariki. Lakini yule ndugu alisema kwamba hangependa kuoa mke mwingine na akamwambia Boazi akomboe lile shamba. Na kwa furaha kuu, Boazi akamaliza kukomboa Ruthuu na lile shamba.
Baadaye Boazi na Ruthuu walizaa mtoto wa kiume wakamwita Obedi ambaye alimzaa Jese baba ya Daudi. Mwenye kuandika Zaburi.

Kama ulifikiri Boazi alitaka shamba lingine basi wewe ukufuata hadidhi vizuri. Yeye alimpenda Ruthuu na kwahivyo akanunua lile shamba ile akapate mke.

Basi tukiangalia angano jipya, tunasema kitabu cha Mathayo 13 pale Yesu alisema ufalme wa mbinguni ni kama kitu cha dhamana ya juu kilichofichwa kwenye shamba, na mtu anapoingudua anafurahi sana. Anauza mali yake yote na kwenda kununua lile shamba. Mathayo 13:44. Je, ukiangalia haya maneno shamba ni nini?.

Katika usomaji wa Bibilia, tunao mpangilio wa maneno na katika misemo. Na hayo maneno humanisha ama huwa na maana moja. Katika ule msemo wa Ngano na chichi zake, alisema kuwa shamba ni dunia. Na kwasababu hiyo, katika maneno tuliyo yasema shamba basi ni dunia.

Swali lifuatalo ni nani yule aliyetoa yote kununua ulimwengu?. Jibu ni Yesu ambaye alitoa maisha yake kukomboa ulimwengu.

Basi hazina iliyofichwa ni ipi? Ni kanisa msichana bikira. Kama Boazi Yesu alitamani bikira ama kanisa lake takatifu ambayo ingepatikana katika ukombozi wa lile shamba ama dunia. Mwili wa kristo ama kanisa ni dhamani yake. Yesu alitupenda sana ata akanunua ulimwengu ili kutukomboa.

Hapo mwanzoni, ulimwengu ulikuwa wa Mungu. Yeye ndiye aliumba ulimwengu. Wakati Mungu alipomuumba mwanadamu akamuweka hapa duniani. Yeye alimpea mwanadamu ulimwengu. Na kutangaza ya kwamba yeye amempa mamlaka juu ya vitu vyote hapa duniani. Adamu alipotenda dhambi aliwekwa minyororo ya shetani kwa hivyo kumuachia ulimwengu shetani katika kitabu cha warumi 6 kina sema ya kwamba yule amejitolea kumtii anakuwa mtumwa wake. Warumi 6:16. Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii mmekuwa watumwa wake. Yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletayo mauti. Ama kwamba ni utumishi wa utii uletao haki. Hii ndiyo sababu uwezi kumlaumu Mungu kwa mambo mabaya yanayotendeka hapa duniani.

Unasikia watu wakisema kama Mungu ni upendo, basi kwanini kuna mateso duniani? Kwanini watoto wanakufa na njaa? Kwanini watu wanakuwa viwete na viziwi? Kwa kuelewa hayo mambo yote ni lazima useme kama Paulo. Kuwa shetani ni mfalme wa huu ulimwengu. Mara nyingi Yesu alimuita shetani mtoto wa mfalme wa huu ulimwengu. Mateso na mashaka yaliyo humu duniani yametokana na yeye. Ukiangalia huoni ulimwengu Mungu aliokusudia lakini unaona ulimwengu uliojaa mateso na dhiki kwa sababu ya kumkataa Mungu. Ulimwengu wa sasa uko chini ya mamlaka ya shetani.

Kama umeamua kumuasi Mungu basi usimlaumu kwa mambo yanayokupata. kwa sababu wewe ndiwe ulimuasi Mungu. Mathayo 6: 9-10. Basi nyinyi salini hivi, Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe, ufalme wako na uje, mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama huko mbinguni.

Ufalme wako na ukija, kondoo na mbwa musituni watalala pamoja, basi jangwa litamea

maua na litakuwa la kupendeza. Na nchi itakuwa ya kuzaa. Kutakuwa hakuna machozi, uchungu wala kifo. Vipofu wataona na viwete wataruka kama dama na bubu wataimba sifa zake Mungu. Taifa alitapigana na taifa lingine wala awatajifundisha vita. ISAIYA 2:4

Bwana anasema hivi, gharama ama pesa zinazotumiwa kwa vita zitawekwa kwa gharama ya ukulima. Ndiyo sababu tunaomba ufalme wako na uje. Yesu alipokuwa humu duniani madhumuni yake ilikuwa ni kukomboa ulimwengu. Sababu ya Yesu kufa hapa duniani, ni kukomboa ulimwengu. Luka 19:10. Kwa kuwa mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilicho potea.
Pia akasema katika Yohana 3: 17, maana Mungu alimtuma mwana ulimwenguni ili ulimwengu uokolewe kupitia yeye. Hii ndiyo sababu maalumu akafanyika mwanadamu ili akawe wa ukoo ama jamii ya binadamu. Ili akawe “goel” Ama mkombozi wa jamii.

Basi shetani alipogundua haya, akachukua Yesu baada ya kupatizwa na kujazwa na Roho mtakatifu na baada ya kufunga kwa siku arubaini, shetani akampeleka mlimani juu, Akamuonyesha ufalme wote wa dunia hii na utukufu ulioko ndani yake. Na shetani akamwambia Yesu, Luka 4:6 . Ibilisi akamwambia, nitakupa wewe enzi hii yote, na fahari yote kwa kuwa imo mikononi mwangu, nami humpa yeyote kama nipendavyo. Yesu hakupingana na shetani alijua mwanadamu amedanganywa na kupewa ulimwengu wote.

Katika kitabu cha Yohana, Yesu akasema mwivi haji ila kuiba na kuchinja na kuharibu. Mimi nilikuja ili mimi na wewe tuwe na uzima kisha wawe nao tele. Yohana 10:10. Mungu amefanya kazi zuri. Basi usimulaumu Mungu kwa mateso yaliyoko duniani. Wale wanao mulaumu Mungu ni wale walioamua kumuasi Mungu na kukubaliana na shetani. Wakati shetani alitaka kumpa Yesu ulimwengu, alitaka kutumia njia rahisi isiyo na msalaba. Ilikuwa ni njia ya kumpoteza Mungu asitumie njia ya msalaba. Shetani alikuwa anampa Yesu njia ya kutosheleka na mambo ya dunia hii ili amuasi Mungu. Ndani ya kitabu cha Mathayo 16, baada ya Petro kukiri Yesu ndiye Messiah. Yesu alikuwa anazungumzia wanafunzi wake juu ya msalaba. Halafu Petro akalia kwa sauti

kuu Mathayo 16: 22-23. Petro akamchukua, akaaza kumkemea akisema hasha bwana haya hayatakupata. Yesu akageuka akamwambia Petro, nenda nyuma yangu shetani. Wewe ukikwanzo kwangu maana uyajui ya Mungu bali ya shetani.

Shetani angali anawajaribu watu wa Mungu kwa kuwatosheleza, ili wakaache njia za Mungu. Shetani anasema ya kwamba njia ya msalaba aina raha wala kutosheleka katika maisha. Shetani anasema ya kwamba, kutosheleka kuko ndani ya mali na vitu vya dunia hii. Madawa ya kulevya., Pombe na kufanya usherati. Watu wengi hujikuta kwenye huu mtego. Maana mwanzoni haya mambo hayaonekani mabaya ni mambo matamu na ya kupendeza. Na baadaya utamu unaisha na unajikuta kwenye shimo la giza.

Yesu alimjibu shetani na maandiko, imeandikwa Mathayo 4:10, Ndipo Yesu alimwambia nenda zako shetani maana imeandikwa, msujudie Bwana Mungu wako umwabudu yeye peke yake.
Yesu akatimiza mpango wa Mungu kuokoa ulimwengu kupitia njia ya msalaba. Yesu alilipa deni ya ukombozi. Damu yake msalabani ilituokoa. Petro ametwambia tumeokolewa kutokana na kuishi maisha ya utupu.
1 Petro 1:18-19, Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viaribikavyo, kwa fedha ama dhahabu mpate kutoka katika mwenendo wenu usio faa. Mlipokea kwa baba zenu. Bali kwa damu ya thamani kama ya mwana-kondoo asiye na hila, asiye na waa yaani, Yesu Kristo .

Kwa sababu Yesu ajajitokeza kusema ulimwengu ni wake kwa hivyo shetani anaendelea kutawala ulimwengu. Huu ni ukweli hata hukiangalia yanayo tokea na pia maandiko.
Katika kitabu cha ufunuo wa Yohana 13, hapo tunasema ya kwamba shetani atampa ufalme yule mnyama (mpinga kristo) ambaye anatawala ulimwengu. Ufunuo wa huyo mnyama uko siku za usoni. Kwa hivyo shetani lazima aendelee kutawala ulimwengu mpaka Yesu atakaporudi ndio ushindi wa Kristo utakapopatikana.

Ufunuo wa Yohana 11:15, malaika wa saba akapiga baragumu, pakawa na sauti kuu katika mbingu,zikisema, ufalme wa dunia umekwisha kuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake. Naye anamiliki hata milele na milele.
Katika kitabu cha waefeso, hapa Paulo anatuambia Yesu ndiye urithi wetu. Ili kuleta ukombozi na utawala wake na kwa sifa na utukufu ni kwake. Wefeso 1:14.

Katika kitabu cha Warumi, tunaambiwa kwa maana twajua ya kuwa viumbe vyote pia vinaungua pamoja navyo vina uchungu pamoja hata sasa. Warumi 8:22, viumbe vyote vinagoja kufunuliwa kwa mwana kondoo. Hii ndiyo wokovu wa miili yetu.

Katika ufunuo wa Yohana 4 na 5 tunayo picha zuri ya mpango ulio kamili wa wokovu. Yohana alisema maneno haya. Ufunuo wa yohana 4:1 baada ya hayo naliona, na tazama mlango ukafunguka mbinguni na sauti ile ya kwanza niliyoisikia kama sauti ya baragumu ikinena nami ikisema, panda hata huku nami nitakuonyesha mambo ambayo hayana budi kuweka baada ya hayo.
Mimi naamini anazungumzia juu ya mambo yaliyoundwa hapo nyuma mlango wa 2 na 3. Kitabu cha ufunuo wa Yohana, mambo kuhusu kanisa, ujumbe wa Yesu kwa kanisa ulishuhudiwa na yeye hapa duniani.

Yohana akaendelea, Nami nikaangalia, nikaona mlango uko wazi mbinguni na sauti ya kwanza niliyo isikia ni kama ya baragumu ikiongea nami ikisema kuja hapa nitakuonyesha mambo yatakayotokea baada ya haya.

Yohana anatuambia alikuwa ndani ya roho huku mbinguni. Na kwanza alivutiwa na kiti cha enzi cha Mungu na utukufu wa Mungu. Akaona upinde wa rangi nyingi zikizunguka kiti cha enzi na kabla ya hiyo bahari ya kioo.na pia akaona viti vya enzi ishirini na vine ambavyo wazee ishirini na wane walikaa. Wamevikwa mavazi meupe na juu ya vichwa vyao wamevikwa taji ya dhahabu. Na hawa wenye uhai wane kila mmoja alikuwa na mabawa sita na pande zote na ndani wamejaa macho wala hawakupumzika mchana na usiku wakisema mtakatifu mtakatifu mtakatifu. Bwana Mungu mwenyezi, aliyekuweko na aliyeko na atakayekuja.

Walipokuwa wakimuabudu Mungu, wale wazee ishirini na wane walianguka kifudifudi nyuso zao mbele ya kiti cha enzi cha Mungu na wakarusha taji zao za thahabu mbele ya kioo cha bilauri na kusema ufunuo wa Yohana 4:11, Unasitahili wewe bwana wetu Mungu wetu, kuupokea utukufu na heshima na uweza kwa kuwa wewe ndiwe uliyeviumba vitu vyote, na kwasababu ya mapenzi yako nilikuweko navyo vikaumbwa.

Ukiwa muangalifu na haya maneno ya wazee ishirini na wane, na kusema kuwa Mungu aliumba kila kitu kwa ajili ya raha zake mwenyewe. Na wewe ni mmoja wao. Wengi wanakataa huu ukweli lakini ukweli wa maisha. Wengi hawakubaliani na Mungu ya kwamba aliumba ulimwengu kwa mpango wake mwenyewe. Wengi ufikiria wameonewa. Lakini ukiishi kulingana na mapenzi ya Mungu, utaishi na raha mstarehe na kutosheleka. Lakini ukiishi na kujipendeza wewe mwenyewe, utakuwa kama Solomoni ambaye hakujinyima chochote. Yeye alipata utajiri kuliko wale waliomtangulia, lakini mwisho aliishi maisha ya uchungu. Muhubiri 1:4, Nimeona kazi zote zifanywazo chini ya jua, na tazama, mambo yote ni ubatili na kujilisha upepo. Maisha yake yalikuwa ya utupu kwa sababu haliishi kujipendeza yeye mwenyewe.na hakujua sababu yake yeye kuishi ni mapenzi ya Mungu.

Katika mlango wa tano wa ufunuo, nikaona malaika mwenye nguvu akihubiri kwa sauti kuu. Ninani anayestahili kukifungua kitabu na kuzifunja mihuri zake? Ufunuo 5:2, Yohana alianza kulia alipongudua kwamba hakuna mbinguni, duniani na hata baharini mtu ambaye angefungua kitabu na kuvunja mihuri zake. Kwanini hiki kitabu kilikuwa na uzito gani mpaka Yohana akalia wakati hakukuwa na mtu wa kukifungua?

Ndiyo maana cheti cha umiliki wa dunia kilicho chapishwa miaka 6,000 iliyopita. Naye Adamu akauza hiki cheti kwa shetani kwa mambo machafu na dhambi. Na kama hakupatikani mtu wa kukikomboa cheti hiki basi ulimwengu utakuwa wa shetani milele na milele. Mfano mzuri ni wakati Boazi alikomboa lile shamba na akamuoa Ruthu. Na kuonyesha umiliki mpya kupitia mkombozi.
Haya maneno yalikuwa mazito sana mpaka Yohana akalia lakini mmoja wa wale wazee

karibu akasema, Ufunuo 5:5; usilie tazama, simba aliyewakambila ya Yuda Jina la Daudi yeye ameshinda apate kukifungua kile kitabu na kuvuja zile mihuri zake saba.

Yohana alingeuka na kumuona. Je, wewe ushawaza itakuwaje kumuona Yesu mara ya kwanza?. Paulo anatwambia ya kwamba saa hizi tunamuona Yesu kupitia Roho Mtakatifu. Lakini tutamuona uso kwa uso. Inaonekana Yesu. Huu ni ukweli maana maandiko yanashuhudia haya.

ISAYA 52 na 53 inasema kwamba wale waliomuona walipigwa na mshangao kwa sababu uso wake ulingaa sikama wa binadamu.

Kumbuka Yesu alipokuwa mbele ya potio Pilato akijaribiwa, walimfunika uso na kitambaa na kuanza kumpiga. Wakampiga na mijeledi. Isaya alisema kuwa tulificha nyuso zetu mbele ya Mungu. Kwa hivyo kuficha nyuso zetu ni kuamanisha tulio na kitu kinachong'aa ama cha kuogovya.

Isaya anaendelea kutukubusha Isaya 53:5. Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu. Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake.na kupigwa kwake sisi tumepona.

Isaya 53:7 anasema, Aliona, lakini alinyenyekea wala hakufunua kinywa chake kama mwana kondoo ambaye anapelekwa machinjoni. Na kama vile kondoo anyamazavyo mbele yao wakatoa manyoya yake. Naam hakufunua kinywa chake. Je, kwa muda tutaona alama za mateso yake? Kama vile Yohana anavyosema.

Ufunuo 5:6, Nikaona katikati ya kile kiti cha enzi na wale wenye uhai wane na katikati ya wale wazee mwanakondoo amesimama alikuwa kana kwamba amechinjwa. Mwenye pembe saba na macho saba ambazo ni roho saba za Mungu zilizotumwa katika dunia yote.

Tunajua ya kwamba atakapofufuka atakuwa na zile alama kwa mwili wake ambazo alipata msalabani kama vile alimwambia tomaso, nyosha kidole chako hapa na uangalie mikono yangu na uweke mikono yako hapa na uingize upande wa mbavu zangu. Yohana 20:27.

Zakaria 13:6 na mtu atamwambia jeraha hizi ulizo nazo kati ya mikono yako ni nini?.

Naye atajibu ni Jeraha nilizotiwa katika nyumba ya rafiki yangu.

Hata hivyo Yohana alimuona kama kondoo amechinjwa akichukua kile kitabu kutoka kwa yule aliye keti kiti cha enzi. Na anapochukua kile kitabu wale wazee ishirini na

wane wanakuja na bakuli za dhahabu zilizojaa manukato na maombi ya watakatifu na ya kotolewa kama dhabihu mbele ya enzi ya Mungu.

Je, wewe ushaomba ufalme wako na uje. Mapenzi yako yatendeke hapo duniani kama uko mbinguni. Wakati umefika wa kuleta haya maombi mbele ya Mungu. Na tunaambiwa, walianza kuimba wimbo mpya.

Ufunuo 5:9, nao waimba wimbo mpya wakisema wastahili wewe kukitwaa hicho kitabu na kuzifungua mihuri zake. kwa kuwa ulichinjwa ukanunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila n lugha na jamaa mataifa. Wale walio okoka ndio wanaweza kuimba wimbo huu.

Hata malaika wanaimba wimbo huu, na hapo mamillioni na mamillioni wana hungana kusema haya maneno.

Ufunuo 5:12 wakasema na sauti kuu. Anastahili mwana kondoo aliyechinjwa, kupokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na baraka.

Tukiwaza juu ya ukombozi, lazima tufikirie juu ya msalaba na mateso. Yesu alipokea msalabani ili akatukomboe kutokana na minyororo ya shetani na dhambi. Na atakufanya wana ili tukatawale na yeye na kushiriki na yeye furaha na maajabu ya upendo wake na ufalme wake katika nchi mpya.

Paulo akasema Warumi 8:31. Basi tuseme nini juu ya haya? Mungu akiwa upande wetu, ni nani aliyejuu yetu? Basi haya nimaneno mazito. Kile tunastahili kufanya ni kumsujudia ndani ya mioyo yetu na kumuabudu kwa roho na kweli.